

SAGCOT
SOUTHERN AGRICULTURAL GROWTH CORRIDOR OF TANZANIA

# Ubia Mkakati wa Viazi Mviringo

## Muhtasari

Nchini Tanzania, viazi mviringo (Solanum tuberosum) wakati mwingine huitwa (Viazi Ulaya), ikiimaanisha vina asili ya kutoa nje ya nchi hii yaani Ulaya au (Viazi mviringo) kutofautisha na viazi vitamu (SAGCOT, 2018). Viazi mviringo ni miongoni mwa mazao makuu kumi ya chakula nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Wizara ya Kilimo kuna wazalishaji zaidi ya 173,772 (MoA, 2017) wanaojishughulisha na uzalishaji wa viazi mviringo ambao wengi kati yao ni Wakulima wadogo. Kiasi kikubwa cha viazi mviringo vinazalishwa katika ukanda ya nyanda za juu kusini unaojumuisha mikoa ya; Njombe, Mbeya, Songwe na Iringa (ukanda wa SAGCOT). Kwa mujibu wa takwimu kutoka Wizara ya Kilimo (MoA, 2019), jumla ya tani za ujazo 337,803 za viazi mviringo zilizalishwa nchini kwenye msimu wa mazao wa mwaka 2018/19, kati ya hizo, tani za ujazo 282,404 asilimia (83%) ya uzalishaji wote vilitoka Nyanda za Juu Kusini. Mkoa wa Mbeya ndio unaoongoza kwa uzalishaji wa viazi mviringo nchini kwa asilimia (49.8%), ukifuatiwa na mkoa wa Njombe asilimia (19%), mkoa wa Iringa asilimia (10.8%) na mkoa wa Songwe asilimia (3.9%) katika msimu wa mazao wa mwaka 2018/19. Kwa ujumla, asilimia (83%) ya viazi mviringo viliyozalishwa nchini vilitoka ukanda wa SAGCOT.

## Wadau muhimu wa Ubia Mkakati wa Viazi Mviringo

- Wizara ya Kilimo
- Mamlaka ya Serikali za mitaa na Sekretarieti za Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini
- Chuo cha Utafiti wa Kilimo (TARI) - Uyole
- Ubalozi wa Ufalme wa Norway
- Ubalozi wa Ufalme wa Netherland
- USAID
- AGRA
- CIP
- Kilimo Trust
- Centre for Development of Potato in Tanzania (CD PIT)
- Grimme
- Yara
- Europlant
- TOSCI
- HZPC
- Bayer Crop Science
- Silverlands Tanzania Ltd
- Tanzanice Agrofoods Ltd
- CRDB Bank
- National Microfinance Bank (NMB)

## Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT)

Mpango wa SAGCOT ni ubia kati ya sekta ya umma na binafsi unaolenga kuchochea Uwekezaji kwenye Kilimo biashara katika ukanda wa kusini mwa Tanzania. Kituo cha SAGCOT kinafanya kazi kama dalali wa ubia na kitovu cha habari kwa wabia wa SAGCOT katika kuwezesha uwekezeshaji kwenye minyororo ya thamani inayoshirikisha jamii na kuzingatia uhifadhi endelevu wa mazingira. Kituo cha SAGCOT kinashiriki kikamilifu kukuza na kuwezesha kutokana na Matukio makuu na yanayoweza kupanua shughuli hizi.

## Nini kinasabisha ubia wa viazi mviringo kuwa ubia mkakati?

- **Kuimarika kwa usalama wa chakula na kubadilisha hali ya maisha katika kaya.** Ubia Mkakati wa Viazi Mviringo unalenga kuongeza mara mbili tija ya uzalishaji na kuongeza mara tatu faida kwa Wakulima wa viazi mviringo katika ukanda wa SAGCOT.
- **Kutafuta masuluhisho ya kudumu katika mnyororo wa thamani.** Ubia wa Viazi Mviringo ulianzishwa kimkakati ili kujumisha wadau kutoka kila eneo linalohusisha mnyororo huu. Ubia huu husaidia kutatua changamoto mbali mbali kwenye mnyororo wa thamani kwa haraka zaidi.
- **Uwezekano wa kupata huduma za kifedha. kupitia asasi za Wakulima**, kuimarisha ushirika wa Wakulima na kuongeza uelewa na maarifa juu ya usimamizi wa fedha na mifumo ambayo Wakulima wataweza kupata zaidi huduma za kifedha.
- **Uwezekano wa kupata maarifa na teknolojia.** kupitia kuitisha mikutano na huduma zinazowafikia Wakulima wa viazi mviringo wanaweza kupata maarifa juu ya mbinu mpya kabisa za Kilimo bora kama vile teknolojia ya kupima udongo na matumizi ya chokaa.
- **Kuitisha wabia.** Wadau wa viazi mviringo walikutana na kujadiliana juu ya visa vitatu vya biashara ambavyo vitasaidia ukuaji wa mnyororo wa thamani wa viazi mviringo kwenye ukanda wa SAGCOT. Kuna haja ya kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za viazi mviringo, kuanzisha asasi ya viazi mviringo na kuwepo kwa muundo mzuri wa masoko yanayouza viazi vyenye ubora wa hali ya juu.
- **Kuimarisha upatikanaji na uwezo wa kupata mbegu bora za viazi mviringo.** Wakulima wazaliashaji 13 wanaozalisha mbegu wameshafanyiwa tathmini kwa kuwapa vibali. Wakulima 8 wameshafuzu mafunzo na wameshaanza uzalishaji wa mbegu chini ya usimamizi wa CD – PIT, TARI na TOSCI. Wakulima hawa wanamiliki mashamba yenye ukubwa wa kuanzia ekari 10 mpaka ekari 40. Wazalishaji wa mbegu waliopewa vibali watasaidia katika kuongeza upatikanaji na ufikiwaji wa mbegu bora za viazi mviringo kwa wakulima wadogo.
- **Kuonyesha athari chanya za kimazingira.** Wabia watafanya kazi kushirikiana na wakulima kuhakikisha kuwa wanawajibu wa kusimamia rasilimali. CD PIT imeonyesha kuwa mkulima anaweza kuzalisha mpaka tani 59 za viazi mviringo katika hekta moja kwa kutumia aina mpya za mbegu ambazo zimetambulishwa nchini. Hii itaongeza uzalishaji kwa ekari, kuongeza kipato cha Wakulima na kuweza kuhimili ushindani kwenye soko.

## Matokeo jumuishi na endelevu

Kwa kuongezea kama ni chanzo muhimu cha nishati, viazi vina tindikali aina ya amino na vitamin. Vinastawi vizuri kwenye maeneo yenye baridi na nyanda za juu za kitropiki zenye hewa baridi, maeneo ambayo yana idadi kubwa ya watu. Kuwekeza kwenye viazi ni fursa ya kusaidia mahitaji ya lishe kwa ajili ya idadi ya watu wanaoongezeka kwa kasi kote vijijini na mijini – na kusaidia kutoa fursa za uzalishaji kipato kwa Wakulima wa viazi vijijini. Zaidi ya hayo, viazi vimetoa ajira kwa vijana ambao wanafanya biashara ya viazi kwenye mitaa ya maeneo yaliyoko mijini.

## Changamoto muhimu

Kwa sasa, kiwango cha uzalishaji wa viazi katika ukanda wa SAGCOT (Njombe, Iringa, Mbeya na Songwe) Njombe ni ya tatu kwa uwezo wa kuzalisha, sababu kubwa ikiwa ni upatikanaji mdogo na matumizi madogo ya mbegu bora, vilevile uelewa mdogo juu ya kutumia mbimu bora za kilimo. Sababu hizi - pamoja miundo dhaifu ya soko, vipimo visivyo vya uzito vinavyokosa kuwa sahihi, upungufu shughuli za kuongeza thamani na ukosefu wa mbinu za kukuza za zao la viazi – vinachangia kupunguza faida ya zao la viazi kwa Wakulima wadogo. Kukabiliana na changamoto hizi, Ubia wa Viazi unaweka nguvu zaidi kwa rasilimali zake na maarifa kujenga masuluhisho kwa kutambulisha mbegu zenye ubora wa juu na utumiaji wa nyenzo za kisasa katika upandaji na uvunaji viazi. Kupitia jukwaa hili la mashauriano, wabia wanaweza kutoa mafunzo na kuonyesha kwenye jamii kusaidia Wakulima watumie hizi teknolojia mpya za Kilimo cha viazi.

Ili kuwa na mbinu jumuishi kwenye mnyororo wa thamani, ubia unaalika wasio wanachama kujiunga, hasa kwa wale wanaojishughulisha katika uchakataji, uzaji wa nyenzo za Kilimo kwa Wakulima wadogo, wabobezi na wafanyabishara wengine katika soko la viazi.

### Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia:


SAGCOT Centre Limited

Gholofa ya 5, Jengo la Ikon
Barabara ya Bains, Masaki
S.L.P 80945
Dar es Salaam, Tanzania

**Simu:** +255 22 260 1024
+255 22 260 0146
**Faxi:** +255 22 260 2368

**Barua Pepe:** info@sagcot.co.tz
**Tovuti:** www.sagcot.co.tz


